

## KUKU WA KIENYEJI ANA FAIDA, RAHISI KUGUGA

**Hosea Joseph**

JITIHADA za mtu binafsi zinaweza kumwezesha kufikia mafanikio ikiwa atakuwa na malengo.

Kwa kulitambua hilo wapo baadhi ya watu ambao licha ya kufanya kazi za kuajiriwa bado wanajishughulisha na kazi nyingine za kujiongezea kipato ili wafikie malengo fulani ya mafanikio zaidi.

Katika mahojiano na mfugaji kuku kutoka katika Kituo cha Huduma ya Mifugo kilichopo Mbezi jijini Dar es Salaam cha Luis Agrovet Centre, Festo Mallya anabainisha kuwa mazao makubwa ya kuku wa asili ni nyama na mayai.

Anasema mara nyingi kuku wa asili walikuwa wanafugwa katika maeneo ya vijijini ambapo katika siku za hivi karibuni umekuwepo mwamko mkubwa kwa watu waishio mijini kwa kujaribu kufuga kuku wa asili kama sehemu ya kujiongezea kipato na kujipatia kitoweo kwa ajili ya familia.

Mallya anasema katika harakati za kupambana na umaskini, kuku wa asili wamechukua nafasi kubwa kutokana na urahisi wake wa kufugwa ikilinganishwa na kuku wa kisasa.

Hivyo Mallya anasema yapo mahitaji muhimu katika ufugaji wa kuku wa asili ambayo kabla ya kuanza kufuga kuku unapaswa uzingatie.

“Elimu ya ufugaji wa kuku ni muhimu kwa kuwa mfugaji anapaswa kupata maelekezo mapana kabla ya kufuga kuku hii ni pamoja na kujua lishe bora, utunzaji wa mazao ya kuku kama mayai pamoja na kutambua na kupambana na magonjwa ya kuu,” anasema Mallya.

Mallya anasema mfugaji anapaswa kufahamu namna ya kutunza kumbukumbu zake za mradi wa kuku ili kufikia mafanikio zaidi, mafunzo ambayo anasema wanayatoa katika kituo chao kwa mtu mmoja mmoja au vikundi.

Anasema mfugaji anapaswa kutambua aina bora ya kuku wa kienyeji ili kumwezesha kufikia malengo aliyokusudia wakati wa ufugaji ambapo ili mfugaji afikie malengo anashauriwa kuchagua kuku bora wa kufuga.

“Kuku wa asili wanazo sifa mbalimbali, mfano sifa za kukua haraka na kuzalisha nyama au mayai kwa wingi, uwezo wa kustahimili magonjwa na kuishi katika mazingira magunu pamoja na uwezo wa kujikinga na maadui,” anasema.

Mallya anasema kuwa ili mfugaji aweze kuweka malengo yake katika vitendo hana budi kutambua uwezo wake kimtaji, kwakuwa mtaji ni pamoja na fedha za kufanya manunuzi mbalimbali pamoja na vitendea kazi.

Mallya anasema upo umuhimu kwa mfugaji kuwa na eneo la kufugia kuku kwa kuchagua eneo kulingana na mahitaji ya mahitaji yake ili kuendana na hali halisi ya mifugo anayotaka kufuga.

“Luis Agrovet Centre inamsaidia mfugaji au kikundi cha ufgaji katika kumwelekeza namna ya kupata mtaji kwa kumpa ushauri wa kitaalamu kutokana na sisi wataalamu wenyewe kuwa wafugaji,” anasema Mallya.

Mallya anasema kupitia kituo chao wameweza kuongeza idadi kubwa ya uzalishaji wa kuku ambapo wamewawezesha zaidi ya watu 11,000 kufuga kuku ambao wanawasaidia kukidhi mahitaji yao.

Pia anasema ili kufikia malengo kila mmoja anapaswa kujihusisha na shughuli nyingine za uzalishaji kutokana na kupanda kwa gharama za maisha kila kukicha ili kuendana na hali halisi iliyopo.

“Nitoe wito kwa wanajamii wote wenyewe uwezo wa kufuga mifugo ya aina yoyote wasiogope kwani ina faida kubwa kwa maendeleo yao binafsi na jamii yao inayowazunguka katika kukidhi mahitaji ya mboga,” anasema.

Anasema yapo mambo mengi anayojivunia kutokana na ufgaji ikiwamo kuwasaidia watu kufikia mafanikio kupitia ufgaji wa kuku na mifugo mingine, jambo analoona ni faraja kwake.

“Wapo baadhi ya wateja wetu ambao nao wana uwezo wa kufuga kuku wengi ambapo wanazalisha kuku wa nyama na mayai kwa wingi, kwa mfano wapo ambao wana uwezo wa kukusanya mayai zaidi ya 400 kwa siku kutokana na mifugo yao hivyo kupata faida kubwa,” anasema Mallya.

Kutokana na hali hiyo, Mallya anahimiza jamii kujihusisha na ufgaji wa aina zote bila kubagua kutokana na hali halisi ya urahisi wa ufgaji mdogo mdogo na faida zake kulingana na jinsi anavyofahamu.